

TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
SHULE YA SEKONDARI UDORO

S. L. P 92,
HAI.
0754 804957
15/12/2020

Kumb Na. UDO/SS/SF.8/GSC/2021

JINA LA MWANAFUNZI
S. L. P
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UDORO WILAYA YA
HAI MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.

1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na Kidato cha KWANZA katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Udoro ipo katika Kata ya Romu Kijiji cha Kimira Kitongoji cha Udoro, Jirani na shule ya Msingi Kishare.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. Shule itafunguliwa tarehe 06/1/2021 saa 2:00 asubuhi. Mwanafunzi asije peke yake. Mzazi atatakiwa kukabidhi fomu zilizoorodheshwa kipegele namba nne na kutia saina sehemu inayohusika. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 20/01/2021.

2.2. SARE ZA SHULE.

- i) WASICHANA: Sketi mbili zenye Marinda kumi na sita, nane nyuma na nane mbele urefu wake uwe chini ya goti katikati ya ugoko wa mguu Belti la sketi liwe na upana wa inchi 2 ½, Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi, viatu vyeusi pea mbili, (vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi) na soksi nyeupe jozi mbili (2), kwa binti wa Kiislamu, "Shungi" inaruhusiwa, iwe nyeupe na iwe ndefu kiasi cha kufunika kongo mbili za mikono akisimama (isifunike viganja vya mikono)
- ii) WAVULANA: Suruali mbili zenye marinda mawili mbele na "turn up" mashati mawili meupe yenye mikono mifupi, soksi nyeupe pea mbili, viatu vyeusi vya kufunga na kamba pea mbili (visivyo na visigino virefu)

NB:

- Kwa rangi na aina ya kitambaa; angalia kitambaa kilichoambatanishwa
- Nasisitiza mwanafunzi anunuliwe T-shirt nyeupe za kuvaa ndani ya shati na sio za rangi ndani ya shati jeupe.

- iii) SWETA: Ni ya mikono mirefu yenye shingo ya "V" mbele. Rangi ya sweta ni ile ya sketi/suruali.
- iv) NGUO ZA MICHEZO: Kila mmoja aje na jezi ya michezo yenye rangi ya blue (kaptula na fulana) raba/viatu vya michezo na soksi ndefu vyote rangi ya blue.

2.3. MAHITAJI YA DARASANI.

- Daftari "Counter book quire II na kuendelea" idadi ziwe Kumi (10)
- Daftari kubwa za kawaida kwa ajili ya mazoezi ya juma kwa kila somo ziwe 9
- Kalamu, penseli, vifutio, rula na kichongeoo.
- Mathematical set (Kofa/Oxford)
- Mfuko/Bag imara wa/la kubebea madaftari.
- Oxford Disctionary (ENGLISH – ENGLISH)
- Mathematical table (4 figure)
- Mche wa mti ulioandaliwa kitaalamu kwenye kitalu cha miti.
- Graph paper- Kitabu kimoja

- 2.4. Chakula cha wanafunzi katika shule za kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani kila siku ya shule, pamoja na matibabu ya mwanafunzi ni jukumu la mzazi. Pia mahitaji mengine yote ya kibinadamu kwa wasichana na wavulana. Haya ni maagizo ya Serikali. Hivyo kutakuwa na kikao cha wazazi wote mwezi Januari 2021 kitakacho endeshwa na kamati ya chakula ili kuweka utaratibu wa kuwapatia wanafunzi wote uji na chakula cha mchana.

MUHIMU:

Shule ya Sekondari Udoro inatekelea agizo la serikali la kila mwanafunzi kupanda mti wake tangu mwaka 2015. Kwa sasa tayari tunayo miti iliyoota 315 inayomilikiwa na wanafunzi wa Kidato cha II, III & IV. Hivyo kila mwanafunzi atakayejiunga na Kidato cha Kwanza – 2021 atapaswa kuja na miche ya miti iliyoandaliwa kitaalamu katika vitalu vya miti kama ifuatavyo:-

- i) Wavulana wote miche ya krevelia
- ii) Wasichana Kishare – miche ya michungwa
- iii) Wasichana wa Tolu – miche ya Parachichi
- iv) Wasichana wa Mudio – miche ya miembe
- v) Mudio Islamic – miche ya limao

Ili kurahisisha utunzaji wa miti hiyo pamoja na mazingira ya shule wavulana wote walete majembe yenye mipini na wasichana walete ndoo ndogo na fagio la chelewa refu lenye mshikio wa mti kudumisha usafi wa mazingira na viunga vya shule. (vifaa hivi ni mali ya mwanao na atapatiwa sehemu salama yakuvihifadhi)

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII .

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 2005. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye Jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na upewe nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, waalimu wako, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- i) Kutunza mali za umma.

NB:

Nakala ya maandishi ya sheria za shule ni kama zilivyo kwenye fomu A iliyoambatanishwa. Mwanafunzi aitunze ili aweze kujikumbusha mara kwa mara.

4.0. Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa kwa Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii inakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni Fomu C.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai - Fomu B.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule – Fomu A.

5.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
J. B. KAVISHE
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
SHULE YA SEKONDARI UDORO

SHERIA ZA SHULE

1. Ni marufuku Mwanafunzi kupigana na mwenzake
2. Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana na kucha/nywele ndefu, kupaka rangi kwenye kucha wala kwenye nywele pia ni marufuku kuweka dawa
3. Ni marufuku kutumia lugha chafu (matusi), kutukana wengine, wanakijiji au watumishi
4. Vazi la shule livaliwe wakati wote mwanafunzi awapo shuleni au kwenye safari rasmi za shule
5. Mwanafunzi anawajibika kufuata ratiba ya shule na kutekeleza yote yaliyopangwa kufuatana na nyakati zake. Kelele madarasani na kupayuka ni dalili ya umaskini wa akili
6. Mwanafunzi awe msafi kimwili na kimazingira
7. Mwanafunzi atii walezi wake, viongozi wa wanafunzi, kengele au wito. Wakati wowote ni muhimu kuwahi mapema mahali unapotakiwa.
8. Mwanafunzi atunze mali ya shule na ya wenzie, wizi, uzembe na udanganyifu ni makosa makubwa sana
9. Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo, kufanya mazoezi na mitihani bila kukosa
10. Kila mwanafunzi afahamu ameingia hapa kujifunza na kujilea katika utu bora, kuchukua madaraka ya kujenga, kulinda na kulea Taifa hili leo na siku zote, hivyo ni muhimu mwanafunzi Ajiheshimu, Ajifunze na kufanya kazi kwa bidii hapa hakuna NAFASI YA KUPIGA UVIVU.

NB: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI.

- (a) Wizi
- (b) Uasherati, ubakaji na ushoga
- (c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
- (d) Uvutaji wa bangi na ugoro
- (e) Makosa ya jinai
- (f) Kupigana au kupiga
- (g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (h) Kudharau Bendera ya Taifa
- (i) Kuoja au kuolewa
- (j) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
- (k) Kutoa mimba
- (l) Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu
- (m) Kukataa adhabu kwa makusudi (ya viboko na nyinginezo)
- (n) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

.....
J. B. KAVISHE
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
SHULE YA SEKONDARI UDORO
S. L. P 92,
HAI.

KUKUBALI SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

JINA LA MWANAFUNZI

TAREHE YA KUZALIWA

JINA LA MZAZI/MLEZI

KAZI YA MZAZI/MLEZI

UHUSIANO NA MLEZI HUYO (MJOMBA, KAKA n.k).....

ANAPOISHI MWANAFUNZI

KATA KIJJI KITONGOJI

KIAPPO CHA UTII

Mimi Nikiwa mwanafunzi wa shule hii, nakubali kuwa, umma wa nchi hii ya Tanzania ndio ulionipa nafasi hii maalum ya masomo, ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi katika maendeleo. Hivyo basi, ninaahidi kwamba, nitajibidisha wakati wote niwapo hapa shuleni na hata nimalizapo masomo yangu. Ili kutimiza shabaha hiyo, ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa, nitatii sheria zote za shule na amri zote nitakazopewa na waalimu wangu. Nikiwa na malalamiko au maoni nitayapeleka kwa viongozi wa shule au waalimu kufuatana na utaratibu uliowekwa.

SAHIHI TAREHE

AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi wa Box Simu namba.

Nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi Naahidi kutimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyu, kwa kumlipia malipo yote yanayotakiwa shuleni pamoja na kumlea kimaadili awapo nyumbani. Endapo atakiuka mojawapo ya sheria za shule au maagizo ya waalimu, basi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake. Pia namuidhinisha Bw/Bi Ambaye ni wangu (taja uhusiano) kuniwakilisha inapobidi. Sahihi ya mzazi

Mimi J. B. KAVISHE

Nikiwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Udoro, naahidi kutimiza wajibu wangu wa kumfundisha na kumlea mwanafunzi huyu kwa uaminifu wote kufuatana na sheria na kanuni za kazi yangu

Sahihi Tarehe

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI UDORO.

HAI DISTRICT COUNCIL
UDORO SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 92
HAI

To medical Officer
.....
.....

Please examine

..... for her/his fitness as a
student in the following areas (to be filled by medical officer)

- 1. Eyesight
- 2. Hearing
- 3. Specimen i) Stool
- ii) Urine
- iii) Blood
- 4. Asthma/Tuberculosis
- 5. Pregnancy (for ladies only)
- 6. Other diseases

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above and consider that he/she is physical fit/unfit *to pursue
Secondary Education

Signature

Designation station

Date Office stamp